# KUKUA KIROHO

UKRISTO NI MTINDO WA MAISHA, JIFUNZE JINSI YA KUWA MKRISTO WA HAPA DUNIANI

TOLEO LA 002 DISEMBA 2025 JARIDA MTANDAO - BURE

# IKIWA WATU WANGU...

JIFUNZE MATUMIZI SAHIHI YA MSTARI HUU, ILI UTUMIKE NA KUWA BARAKA KWENYE MAISHA YAKO YA UKRISTO.



## VIPINDI NA ZAMA

Kuna zama 4 na vipindi viwili ndani ya biblia...jifunze.

## MATUMIZI

Utofauti wa matumizi ya mstari kwa agano la kale na wakati wa sasa.

Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; **basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.** '

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 02 |
| Mazingira | 03 |
| Msingi wake | 07 |
| Matumizi | 10 |
| Mambo ya kujifunza | 19 |
| Kukua kiroho | 20 |

# Utangulizi

“ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.”
2 Nya 7:14 SUV

Huu ni mstari ambao umekuwa unatumika sana zama ama kipindi ambacho watu wanakuwa kwenye changamoto, hii imekuwa ni kasumba kutumika bila kuangalia mzizi wa mstari husika ili kutambua , namna nzuri ya kurithi na kumiliki ahadi hizi sio kwa kulisoma neno na kuchukua mstari tu bali kwa kuelewa maana na mazingira yake ili matumizi yake yawe na matokeo chanya kwenye imani zetu.

Ni ukweli kuwa maombi yasiyojibiwa huwa yanaleta changamoto kwenye imani kwakuwa sote ni binadamu lazima kukumbuka hilo lakini swali la msingi zaidi ni kwamba tumefuata taratibu zote za kupokea ahadi au tumetumia uhitaji tu ili kupokea?

*Somo letu leo*

Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." 2 Nya 7:14 SUV

# MAZINGIRA

Huu ni mstari pendwa kwa watu wengi sana na unatumika sana katika nyakati ngumu na zile ambazo zinahusisha halaiki, ama changamoto ya kikundi hii ikimaanisha kuanzia familia hadi nchi, ni muhimu sana kuelewa msingi wake ili tunapoomba iwe kwa kumaanisha na kuendana na mstari huu, hatua za kuanza kuuelewa mstari huu ni muhimu sana kutambua **mazingira** ya uandishi wake ili kupata picha nzuri yenye maelezo yaliyokamilika.

Kabla ya kwenda kuangalia mwandishi na nyakati ni vyema kuielewa biblia kwanza ili kutambua uandishi wake ulifanyika katika kipindi gani, Kwenye biblia kuna zama 4 na vipindi viwili, ambavyo vimetambulishwa kwa nyakati tofauti.

**Zama ndani ya biblia ni**

1. Kabla ya sheria
2. Ndani ya sheria
3. Kipindi cha Kristo
4. Baada ya Kristo kuondoka

**Somo**

**2 NYAK 7 : 14**

**Vipindi ndani ya biblia ni 2**

- Agano la kale zama 2 za mwanzo
- Agano Jipya zama 2 za mwisho

Ni jambo jema kutambua unapotumia mstari ni kwa kulingana na zama zipi na ikiwa unauleta kwenye zama hizi unashabihiana vipi?, biblia sio ya kuifanya kwa mazoea ila kwa maarifa.

# MAZINGIRA - ZAMA

**Zama za kabla ya sheria** kipindi ambacho kimeandikwa ndani ya biblia kabla ya kipindi cha sheria yaani kabla ya kipindi cha Musa nikimaanisha kipindi cha kina Ibrahimu kabla ya Musa, Mungu alikuwa anatembea na mtu wake kwa ajili ya kutimiza ahadi yake na watu wake ( Israeli) Ibrahimu - Isaka - Yakobo ( israel ) nakuendelea, hadi kipindi cha Yusufu wanaenda Misri kisha baadae wanakaa utumwani.

Kipindi hiki chote kinaitwa kabla ya sheria yaani kabla Mungu hajaweka sheria mama za kuwaongoza watu wake, haimaanishi kulikuwa hakuna kabisa sheria zilikuwepo lakini ni za mtu na Mungu, katika kipindi hiki Mungu alikuwa ni wa mtu zaidi kwa ajili ya watu yaani anamuinua mmoja kwa ajili ya watu wake ambao walikuwa wanaamini Mungu kupitia mtu wake, muunganiko wa Mungu na watu wake ilikuwa ni kupitia mtu husika.

Unapotumia maandiko ya kipindi hicho ni muhimu kutambua Je hakukuwa na maboresho ya hilo andiko huko mbele, na kama kulifanyika maboresho yanasemaje na yanatumikaje kwa zama hizi, lakini ni sahihi kutumia mstari ambao tayari unamaboresho?.

**Baadae zikaja zama za Sheria** kutoka kipindi cha Musa hadi ujio wa Kristo ( kwa ujumla wake kulikuwa na sheria 613 ambazo zilitumika kipindi hiki) Safari ya wana wa Israeli ilitengeneza sheria nyingi wakiwa jangwani hadi kufika nchi ya ahadi lakini pia wakiwa huko sheria ziliendelea kutungwa hadi mwisho wa agano la kale kitabu cha Malaki, lakini hii inaendelea hadi anapokuja Kristo ndio maan kuna muda mafarsayo walimuuliza kama anaijua sheria ya Musa, sababu kilikuwa ni kipindi cha sheria , hivyo pia unapotumia ni muhimu kuangalia hakuna maboresho yake.

# MAZINGIRA – ZAMA

Zama za agano la kale zinaishia hapo na linaanza Agano jipya, baada ya Kristo kuanza kazi tunakihesabu kipindi hicho ni zama mpya kwani zinakuja na mwongozo mpya tofauti na ule wa zamani, tena ukiwa wa juu sana, maana agano la kale lilikuja kupitia wanadamu kamili , lakini sasa agano jipya linaletwa na mwanadamu kamili lakini nafsi ya pili ya Mungu, kwa lugha nyingine ni MUNGU mwenyewe aliamua kushuka ili kurekebisha sehemu zilizobomoka au misingi iliyovunjwa, hebu fikiria umaalum wetu zama hizi kwa Neno mwenyewe kushuka kwa ajili yetu, sasa ukiwa mkristo ni muhimu kujiuliza baadhi ya maswali kama ( Kwanini ni agano jipya? Ni nini hasa maana ya kuwa na agano la kale na agano jipya?)

"Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora. Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili."

**Ebr 8:6-7 SUV**

"Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka."

**Ebr 8:13 SUV**

"Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki."

**Rum 10:4 SUV**

# MAZINGIRA - ZAMA

## ZAMA ZA PILI - KIPINDI CHA TATU

### Kipindi Kristo akiwa duniani.

Zama za pili na kipindi cha tatu zinaanza na utumishi wa Kristo na maboresho ya agano, ambapo imeelezewa zaidi kwenye vitabu vya injili ( *Mathayo, Marko, Luka, na Yohana*), kuzaliwa kwa Yesu hadi anapoondoka na kupaa mbinguni, kuna tufundisha mambo mengi sana na kunaboresha mambo mengi pia hivyo pia unapotaka kutumia maandiko ya zama hizi ni muhimu kutambua waliambiwa akina nani kwa mlengo gani ( Mambo yalibadilika sana kutoka agano la kale ( Damu kwenda Imani, asili moja kwenda dunia nzima) na kadha ni muhimu sana kujua muunganiko.

## ZAMA ZA PILI - KIPINDI CHA NNE

### Baada ya Kristo kuondoka.

Zama Baada ya Kristo inaelezwa zaidi na vitabu baada ya Kristo kupaa mbinguni, wanafunzi na watu kadha wanayaelezea maisha ya wakristo na jinsi walivyoeneza kanisa, katika Agano jipya kuna vitabu 26 na katika hivyo vitabu 16 (17 Ebrania ) ni nyaraka zake mtume Paulo, lakini baada ya Kristo ndio Roho Mtakatifu anatambulishwa hii inamaanisha ni mwendelezo wa maboresho, hivyo ni muhimu kutambua hasa maandiko yanafundisha nini kwa mlengo upi.

**HIVYO MSTARI WA SOMO UKO**

**Zama** ni Agano la kale, **kipindi** ni Kabla ya Sheria.

# MSINGI WAKE

Msingi wa mstari kutoka kitabu cha Mambo ya nyakati 2, ambapo kinamzungumzia Mfalme Suleimani mtoto wa Mfalme Daudi anapofanya mazungumzo na Mungu juu ya watu wake na matukio.

Hii ilikuwa ni sehemu ya 2 ya mahojiano kati ya Suleimani na Mungu. Baada ya Suleimani kukamilisha ujenzi wa hekalu la kuabudia, baada ya kuwa baba yake (Daudi) alikatazwa kulijenga sababu ya damu mikononi mwake.

*"Ndipo Daudi mfalme akasimama kwa miguu yake, akasema, Nisikilizeni, ndugu zangu, na watu wangu; Mimi nalikuwa na nia ya kuijenga nyumba ya kustarehe kwa ajili ya sanduku la agano la BWANA, na kiti cha kuwekea miguu yake cha Mungu wetu; hata nalikuwa nimeweka tayari kwa kujenga. Lakini Mungu akaniambia, Wewe hutajenga nyumba kwa ajili ya jina langu, kwa sababu umekuwa mtu wa vita, nawe umemwaga damu."* ***1 Nya 28:2-3 SUV***

*"Basi ilikuwa moyoni mwake Daudi, baba yangu, kujenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wa Israeli. Lakini BWANA akamwambia Daudi baba yangu, Kwa kuwa ilikuwa moyoni mwako kujenga nyumba kwa jina langu, ulifanya vema kuwaza hivi moyoni mwako; lakini si wewe utakayeijenga nyumba hiyo; ila mwanao atakayetoka katika viuno vyako, yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu."*
***2 Nya 6:7-9 SUV***

# MSINGI WAKE

Hivyo baada ya Suleiman kukamilisha ujenzi wa hekalu ndio anaamua kuliweka wakfu, ili watu wanaokuja wapokee majibu yao kulingana na maombi yao.

Ukisoma 2 Nyakati 6 : Kuanzia mstari wa 12 hadi wa 42 utaona maombi ( Sala ) za Suleimani kwa ajili ya kuliweka wakfu madhabahu na kulizindua hekalu, sasa katika mambo ambayo Suleimani aliomba yafanyike, nitachukua baadhi ya mistari ili kuoanisha na kile ambacho kilijibiwa.

*“Walakini umwangalie mtumwa wako anayoyaomba, na kusihi, Ee BWANA, Mungu wangu, usikie kilio na maombi anayoyaomba mtumwa wako mbele zako; ili macho yako yafumbuke kwa nyumba hii mchana na usiku, mahali uliponena, ndipo utakapoliweka jina lako; usikie maombi atakayoomba mtumwa wako, akikabili mahali hapa. Uyasikie atakayosihi mtumwa wako, na watu wako Israeli, watakapoomba wakikabili mahali hapa; naam, usikie toka makaoni mwako, toka mbinguni, nawe usikiapo, samehe.”* ***2 Nya 6:19-21 SUV***

*“Ikiwa watu wako Israeli wamepigwa mbele ya adui zao, kwa sababu wamekukosa wewe; kama wakirejea kwako, na kulikiri jina lako, wakikuomba na kukusihi nyumbani humu; basi usikie huko mbinguni, ukaisamehe dhambi ya watu wako Israeli, na kuwarejeza tena katika nchi uliyowapa wao na baba zao. Ikiwa mbingu zimefungwa, hata hakuna mvua, kwa sababu wamekukosa wewe; kama wakiomba wakikabili mahali hapa, na kulikiri jina lako, na kuiacha dhambi yao, uwatesapo; basi usikie huko mbinguni, ukaisamehe dhambi ya watumwa wako, na ya watu wako Israeli;*

# MSINGI WAKE

*uwafundishapo njia njema iwapasayo waiendee; ukainyeshee mvua nchi yako, uliyowapa watu wako iwe urithi.”* ***2 Nya 6:24-27 SUV***

*“Wakikukosa, (maana hakuna mtu asiyekosa), hata uwakasirikie, na kuwatia mikononi mwa adui zao, wawahamishe, na kuwachukua mateka mpaka nchi iliyo mbali au iliyo karibu; basi wakikumbuka katika nchi walikohamishwa, na kutubu, na kukusihi katika nchi ya uhamisho wao, wakisema, Tumekosa, tumetenda kwa ukaidi, tumefanya maovu; wakurudiapo kwa mioyo yao yote, na kwa nia zao zote, katika nchi ya uhamisho wao, adui walikowahamisha, wakiomba na kuielekea nchi uliyowapa baba zao, na mji huu uliouchagua, na nyumba hii niliyoijenga kwa jina lako;”* ***2 Nya 6:36-38 SUV***

Hapa ni Suleimani analikuwa anafanya maombi kwa ajili ya uzinduzi wa hekalu lakini akiiweka wakfu madhabahu na anasema mambo ambayo, angetamani yatokee pale ambapo watu wake watakaifikia matokeo yao.

Ndipo sura inayofuata sura ya 7. Mungu anamjibu Suleimani kulingana na maombi yake aliyofanya.

*“BWANA akamtokea Sulemani usiku, akamwambia, Nimesikia uliyoyaomba, na mahali hapa nimejichagulia kuwa nyumba ya dhabihu. Nikizifunga mbingu isiwe mvua, tena nikiamuru nzige kula nchi, au nikiwapelekea watu wangu tauni;”* ***2 Nya 7:12-13 SUV***

# MSINGI WAKE

*“ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao. Sasa macho yangu yatafumbuka, na masikio yangu yatasikiliza maombi ya watu waombao mahali hapa. Maana sasa nimeichagua nyumba hii na kuitakasa, ili kwamba jina langu lipate kuwako huko milele; yatakuwako na macho yangu, na moyo wangu daima.”*
***2 Nya 7:14-16 SUV***

Huu ndio msingi wa mstari huu kwa kumaanisha kuwa yalikuwa ni majibu ya maombi ya Suleimani kutoka kwa Mungu. Ili kuelewa funzo ni vizuri kwanza kuelewa msingi wa neno, hivyo kwa kufuatilia mstari huu ni mwendelezo wa maombi na majibu kati ya Mfalme Suleimani na Mungu.

# MATUMIZI YA MSTARI

Matumizi ya mstari huu yanaendana na sababu nyuma ya maombi yake, kama msingi unavyojieleza hapo awali kuwa yalikuwa ni majibu ya Mungu kwa watu wake iwapo watafanya kama vile Mungu alivyowaagiza basi watasamehewa dhambi zao.

Matumizi yake baada ya kuwa Mungu ameshaikubali madhabahu na hekalu lile inamaanisha ni Mungu kulitimiza neno lake.

*“Ndipo BWANA akaniambia, Umeona vema, kwa maana ninaliangalia neno langu, ili nilitimize.”* ***Yer 1:12 SUV***

Ambapo iwapo wana wa Israeli wangefuata hayo basi Mungu alikuwa anasubiri ili kutimiza neno lake hivyo.

# MATUMIZI YA MSTARI

Hivyo mstari huu ni ahadi ya utimilifu wa matukio dhahaniwa, na nguvu ya madhabahu, matumizi yake tunayatenga katika nyakati mbili ambazo hatuna budi kuelewa na kufanyia kazi kwa kila mstari ili kupata ujumbe mahsusi ndani yake.

1. **Agano la kale**

Kwa agano la kale mstari huu unaonyesha mahusiano mazuri na Mungu yanavyotoa majibu lakini kuonyesha kuwa unaweza kuomba kitu kwa Mungu naye akakubaliana na jambo lako kwa kuwa tu nia yake ni njema na itamrudishia sifa na utukufu, hivyo kwa agano la kale ni mstari unaoonyesha mahusiano ya Mungu na wanadamu kupitia Sulemani lakini pia kuonyesha nia na dhamira safi ya Sulemani kwa watu wake, anapowaombea nguvu ya madhabahu hata ikiwa haijaanza kufanya kazi, aliwafikiria katika udhaifu wao wangeihitaji ili kujisafisha na kusafishwa dhambi zao na akawahi kuweka misingi ili isiwe madhabahu ya ukawaida tu hivyo kuna jambo la kujifunza kupitia hili tunapoweka madhabahu ziwe na sababu na ziwe na nguvu zinenewe mahitaji yake ili isiwe ya ujumla tu.

Lakini upande wa matumizi yake ni kwamba mstari huu hauna matumizi kwa maandishi ila matendo kupitia maelekezo ndani yake, maombi ya Sulemani yalihitaji majibu ya Mungu hivyo alipojibu ahadi lakini kuna mahitaji ya kukamilishwa ili afanye kama Sulemani alivyofikiria hivyo mstari huu kwa agano la kale unaingia kwenye vitendo zaidi ili kupata matokeo, unatumika kama sehemu ya historia ya Mungu na watu wake lakini ukiwa na uhitaji mkubwa wa kufuata kanuni ndani yake.

# MATUMIZI YA MSTARI

1. **Wakati wa sasa.**

mstari huu unapotumika kwa sasa kuna mambo kadhaa ya kuangalia ili kujifunza ukatoe maana na kuwa na nguvu sawa ile iliyofikiriwa katika agano la kale, sio mstari wa kutumia tu kwavile una ahadi ya kuponya hivyo unapohitaji msamaha na kuponywa basi unautumia, watu wengi huukimbilia huu mstari kwa msingi wa mambo mawili

1.Watu wangu kwa maana ya **Wakristo**

2.Wakijinyenyekesha nitawasamehe dhambi yao **( Kusamehewa)**

Hivyo hutumia msingi huo ili kuomba ahadi hii bila kuangalia uhalisia wa mstari wenyewe na mambo ya kuzingatia ili uwe na maana tena kwa wakati huu pia, sasa kwa kuzingatia msingi wa mstari na maboresho ya uhusika na mahusiano na Mungu, Kwanza jambo la kutambua ni kwamba mstari huu unageuka kutoka kwenye madhabahu ambapo ndio msingi wake ilikuwa sehemu Suleimani aliusimika kwenye madhabahu lakini kwa sasa maombi yake sio kwa madhabahu tena kama ilivyokuwa zama hizo sasa ni kwenda na kwenye Imani ambayo Kristo aliiweka kama msingi wa ukristo sasa, hivyo mstari huu kwa zama na nyakati hizi unahitaji vitu viwili

1.Imani

2.Matendo.

# MATUMIZI YA MSTARI

Kwa kuzingatia msingi au mlengo wa mstari huu kwa wakati huu ili kuidai ahadi hii tunatakiwa kwanza kutimiza yale yaliyoandikwa kwenye makubaliano ya ahadi kati ya Mungu na Sulemani kisha ndio tuje tuiombe kwenye maisha yetu ikimaanisha ili tuitumie ahadi hii ni lazima kwanza

1. watajinyenyekesha, **( Kujinyenyekesha)**
2. na kuomba, **( Kuomba)**
3. na kunitafuta uso, **( Kunitafuta uso)**
4. na kuziacha njia zao mbaya; **( Kuziacha njia zao mbaya)**

Haya ni mambo manne yanayobeba nguvu ya mstari huu kabla ya kuiomba ahadi unatakiwa kuyatimiza kwanza, sasa tuangalie moja baada ya jingine.

**1.Kujinyenyekesha.**

Mungu anahitaji unyenyekevu kwake, kwa asilima zote 100, ili uwe wake basi unatakiwa kunyeyekea chini ya mkono wake kwani ni mkuu kuliko yote na vyote, yeye ni mwanzo na mwisho pia ukuu wake unapita vyote hivyo Mungu sio kama anataka useme tu ila utende sio tu kumuamini ila kumuamini na kumtumia kwenye maisha yako ambapo sifa moja ya kuwa wa kwake ni unyenyekevu.

# MATUMIZI YA MSTARI

' 'Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema. Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. '***1 Pet 5:5-8***

Mstari huu unatukumbusha uhitaji wa kunyenyekea na ahadi nyuma ya unyenyekevu lakini na hatari iliyopo nje ya unyenyekevu, hili ni la muhimu sana kulifanya lakini sio hiyo kinyume cha unyenyekevu ni kiburi, na Mungu amesema atawapinga hivyo hata kama una haki ya kupokea ahadi kama unakiburi hauwezi kuipata hii inamaana tayari kwa zama hizi ni jambo la muhimu kujichunguza na kuona ili kuutumia mstari huu je kiburi hakitajwi kwako, lakini kiasi na kukesha je?

Njia nzuri ya kutambua kama kinachotajwa unacho ni kuangalia kinyume chake hivyo ili kujijua ni mnyenyekevu jichunguze kama unacho kiburi, nak ama unacho tambua unakuwa umekosa sifa za kutumia mstari huu, sababu ni mstari ambao tayari una misingi yake.

# MATUMIZI YA MSTARI

**2.Kuomba**

Mungu anarudi kuweka msingi mwingine ni kuomba, maombi ni mawasiliano na Mungu hivyo ni lazima kuongea na Mungu kuhusu shida yako sio kukaa kimya na Mungu aione akuondolee Hapana unatakiwa kutambua mwenyewe na kuomba kulingana na uhitaji wako, lakini kwakuwa tuko zama za baada ya Kristo unatakiwa kuwa na muunganiko mzuri kati yako na Roho Mtakatifu ili kutambua unachotakiwa kuomba kwa ufasaha.

*'Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. '**Rum 8:26***

Hivyo kuomba ni lazima lakini ili maombi yako yasikike unatakiwa kuwa mawasiliano mazuri na Roho Mtakatifu ili akuongoze aina ya maombi lakini na jambo sahihi la kuombea sio kwa mhemko ila kwa uhitaji, ambapo mwongozo wa maombi yapo ya aina 4.

*' Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; '**1 Tim 2:1***

Unatakiwa kufahamu aina ya mawasiliano unayotaka kufanya na Mungu ili usifanye mambo kwa mazoea ila kwa ufahamu hapo ndio unakuja uhitaji wa kutambua maombi ya kusimama na ahadi za mstari ule ni dua, sala, maombezi au shukrani? Hivyo ili kuweza kuomba ahadi nyuma mstari ule ni lazima kuangalia kama unafahamu kuomba? Lakini kama unafahamu kuomba unafahamu tofauti za maombi husika ili usichanganye?.

# MATUMIZI YA MSTARI

**3.Kunitafuta uso.**

Kuutafuta uso wa Mungu ni jambo jingine ambalo watu wengi hushindwa kuelewa maana yake kwa uharaka sababu ya uhalisia wa kuwa uso wa Mungu sio kitu cha kutafutwa kirahisi, maana ya kuutafuta uso wa Mungu inakuja kutokea.

*'Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. '**Mwa 1:26***

Mwanadamu aliumbwa na sura ya Mungu, lakini Mungu ni Roho sasa vilivyoko rohoni vinawezaje kuwa na sura katika ulimwengu wa mwili?, ni hivi mfano wetu ni mwanadamu kuwa na roho maana yake anauwezo wa kuishi kwenye ulimwengu wa roho na mwili, lakini pia kwa sura yetu maana yake mwenye tabia za uungu ndani yake ( kuumba, kuabudiwa, kutawala, hekima, heshima nk) kumbuka hii ilikuwa ni kabla ya mwanadamu kuwa na mwili hivyo kutengeneza matendo ya mwili, hivyo sura ya Mungu ni matendo ama tabia za kiungu ambapo kwenye mstari wetu neno limesema “kunitafuta uso” maana yake ni Kutenda matendo ya kiungu ama yenye tabia za Mungu ndani yake, hapo ikiwa inamaanisha matendo ama tabia zinazoongelewa ni zile ambazo zinamfanya mwanadamu anahesabiwa haki.

*'hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki. '**Gal 2:16***

# MATUMIZI YA MSTARI

Hivyo kuutafuta uso wa Mungu ni kwa kupitia matendo pasipo sheria ambayo unapotenda yamefungwa kwenye kifungo cha kiasi, hivyo hata matendo pasipo sheria pia usifanye kupitiliza Mungu ameweka kiasi kwa kila kitu hata matendo haya pia, hivyo kuutafuta uso wa Mungu ni kwa Kutenda matendo yasiyokuwa ya sheria kwa wingi wake, kisha ndio uende ukadai ahadi iliyoko nyuma ya mstari ule.

**4. na kuziacha njia zao mbaya; ( Kuziacha njia zao mbaya)**

Na jambo la mwisho ili kumiliki ahadi za mstari huu ni kuziacha njia zao mbaya, hii inamaanisha kusimamia amri kuu kutoka kwenye zile amri 10 sasa ni amri 2 tu ambazo zinaondoa njia zote mbaya maana yake ni kuwa na upendo ambao ni asili ya Mungu mwenyewe.

*‘Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. ’* ***Mt 22:37-40***

*‘Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria. ’* ***Rum 13:9-10***

Hivyo kuacha njia mbaya maana yake kuonyesha upendo kwa uhalisia sio kwa kusema ama kwa maneno bali kwa vitendo. '

*Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. '* ***1 Yoh 4:7***

# MATUMIZI YA MSTARI

Hivyo kabla ya kuiomba ahadi ya mstari wa msingi ni lazima kujiona kuwa umeshayakamilisha haya ambayo Mungu aliyakubali na kuiweka ahadi yake ndani yake, kuwa ili awaponye basi ni lazima wafanye kwanza hayo.

Sasa kwa kipindi hicho ilikuwa ni Suleimani kuzindua hekalu lakini maombi yake wakati akiweka wakfu madhabahu, ina maana wengine hawakuwa na ushiriki wa moja kwa moja ila kwa imani na mahusiano binafsi ya Mungu na Sulemani ndio sababu ya kusikilizwa kwa maombi yake, sasa kwa zama hizi za kwetu mstari unaanzia mwisho kwenda mwanzo kwa kuwa wewe unahitaji kutumia ahadi za Sulemani basi unatakiwa kukamilisha kwanza yale ambayo Mungu aliwaagiza wayafanye ili kusamehewa na nchi kuponywa ndio sasa uende kuomba kwa sababu wewe unajua msingi na mahitaji ya ahadi hii.

Jambo jingine kutambua kuhusu ahadi za ndani za biblia nyingi zinakuja na sheria zake ili kukamilika , hivyo unapotaka kutumia angalia ukamilifu wake ulihitaji nini na nini ili kukamilika na sio kama unatumia tu kwa kuwa unaona inafaa kwa uhitaji wako, ni vizuri kutumia mistari hii ya ndani ya biblia lakini hakikisha umetimiza matakwa yake, lakini ni bora zaidi kuwa na mahusiano na Mungu ili upokee ahadi zako na maagano yenye uhalisia na yanayoendana na maisha yako ya kila siku.

# MAMBO YA KUJIFUNZA

1.Sio kila neno(andiko) ni la kutumia kwa sababu umeliona ndani ya biblia, kwanza fuatilia mzizi wake ili uweze kulitumi kwa ufasaha.

2.Nia njema ya Sulemani kwa watu wake, hakuomba kwa ajili yake ila kwa ajili ya watu wake zaidi.

3.Ni jambo jema kuwa na madhabahu lakini umeiombea ifanye nini kwenye maisha yako, usiifanye kwa ukawaida na mazoea ina nguvu zielekeze vizuri ( na ili kuelewa zaidi jinsi alivyoiweka wafkfu soma sura nzima ya 6 na 7)

4.Kutambua kosa na kujirudi ni msingi wa msamaha, Mungu anaonyesha tangu zama ishu sio kusema tu ila kusema na kugeuka na ukatende vile anavyotaka na anatoa mwongozo wa namna ya kutenda, hivyo ukitenda zaidi kama alivyowaelekeza hautahitaji tena ahadi za madhabahu ya Sulemani bali utatengeneza ahadi zako wewe na Mungu kwa kiwango na mahusiano yako na Mungu.

5.Ahadi za ndani ya biblia zimegawanyika katika makundi mengi msingi wa ahadi ni wa muhimu kuliko matokeo yake.

BWANA AKUBARIKI

# Kukua Kiroho

Kukua kiroho ni huduma ya mafundisho, kukuza na kulea imani kwa mkristo, nia na lengo la huduma hii ni kumsaidia asiekuwa mkristo, anaeingia na kuanza kuwa mkristo, alie mkristo ( mchanga  au aliekomaa) kuweza kutambua maana, mafundisho na kujitambua mwenyewe kupitia  mafundisho hayo.

**KUKUA KIROHO NI WAJIBU WA KILA MKRISTO**

'Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu; ' 1 Pet 2:2

' Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, ' 1 Kor 3:1-2

'Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.' Ebr 5:12-14

Mkristo unao wajibu wa kukuza na kupandisha imani yako kutoka utoto uchanga kwenda utu uzima, uwe na imani yenye uwezo wa kupingana na nguvu za giza bila kuomba ila kwa nguvu zake, kuomba bila kukoma haimaanishi muda wote uwe unaomba tu ila muda wote uwe na muunganiko mzuri kati yako na ulimwengu wa roho kupitia Roho Mtakatifu, hivyo ukiwa na muunganiko huo ni sawa na kuwa kwenye maombi muda wote kwani huko kuna UWEZA , Hekima na Maarifa ambavyo vitakusaidia sana kufanikisha mambo yako katika ulimwengu wa mwili.

Karibu tujifunze kwa pamoja, karibu KUKUA KIROHO.

# JARIDA LA KUKUA KIROHO

DISEMBA 2025

**Limeandaliwa na**
Elisha Chuma
*Huduma ya Kukua Kiroho*

kukua kiroho
kukua kiroho
kukuakiroho@echu.co.tz